



ELECTION PROTECTION

866
OUR
VOTE

UPIGAJI KURA SIKU YA UCHAGUZI wa 2022

Tutumie barua pepe: info@movpc.org

Kile Wapiga Kura Wote wa Missouri Wanahitaji Kujua

NITAPIGA KURA WAPI?

Angalia kadi ya upigaji kura kutoka kwa mamlaka ya uchaguzi au piga simu kwa 866-OUR-VOTE ili ufahamu unakoweza kupigia kura. Huenda kituo chako cha kura kikabadilishwa! Wapiga-kura katika baadhi ya maeneo wanaweza kuteua kupiga kura katika vituo kadhaa, kama vile Vituo au Maeneo Makuu ya Kura, lakini wapiga-kura wengine wote wanahitaji kupigia kura katika vituo mahususi vya eneo lao.

VITUO VYA KURA ZINAFUNGULIWA SAA NGAPI?

MAENEO YA KUPIGIA KURA YANAFUNGULIWA SAA kumi na mbili asubuhi hadi saa moja jioni **SIKU YA UCHAGUZI**

UNAHITAJI KUSAFIRI? Piga simu kwa 1-866-OUR-VOTE ili upate usaidizi Bado unaweza kupiga kura hata ikiwa umechelewa mradi uko kwenye foleni ifikapo saa moja jioni na ubaki kwenye foleni.

NINAHITAJI KITAMBULISHO KIPI?

SHERIA MPYA: Ili kupiga kura kawaida Siku ya Uchaguzi au kupiga kura bila kufika kituoni, onyesha **MOJAWAPO** ya vitambulisho hivi: Leseni ya udereva ya Missouri ambayo muda wake haujakwisha au isiyo ya udereva; Kitambulisho cha kijeshi ambacho muda wake haujakwisha, ikiwemo na kitambulisho cha kustaafu; Pasipoti ya Marekani ambayo muda wake haujakwisha; au Kitambulisho kingine cha picha kilichotolewa na serikali ya Marekani au jimbo la Missouri ambacho muda wake haujakwisha au ulikwisha baada ya uchaguzi mkuu wa hivi majuzi. Wapiga-kura wasio na kitambulisho kinachohitajika wanahitaji yafuatayo ili kura zao zihesabiwe: kurejea kituoni na kitambulisho halali cha picha au kuhakikisha saina kwenye bahasha ya kura inalingana na ile iliyo kwenye rekodi za tume ya kura.

Je, una maswali au unahitaji usaidizi? Piga simu au tuma ujumbe

866-OUR-VOTE (866-687-8683)

Gumzo la Mtandaoni: 866OURVOTE.org Huduma za Lugha Mahususi:

Kihispania **888-VE-Y-VOTA** • Lugha za Asia **888-API-VOTE** •

Kiarabu **844-YALLA-US**

1-866-OUR-VOTE



ELECTION PROTECTION

866
OUR
VOTE

JE, NAPASWA KUFANYAJE IKIWA JINA LANGU HALIPO KWENYE SAJILI?

Ikiwa jina lako halipo kwenye orodha ya wapiga-kura katika kituo chako, afisa wa uchaguzi anahitaji kupiga simu kwa mamlaka husika ya kusimamia uchaguzi ili kuthibitisha usajili wako na kukuelekeza kwenye kituo sahihi. Iwapo ulihamia Missouri kutoka kaunti nyingine na hukusasisha usajili wako, huenda ukahitaji kusasisha anwani yako kwenye ofisi ya uchaguzi na upige kura yako hapo. Ikiwa usajili wako hauwezi kuthibitishwa, unaweza kupiga kura kisha itahesabiwa baadaye. Kura za kuhesabiwa baadaye sharti ziwekwe inapostahili.

JE, NAPASWA KUFANYAJE KUTHIBITISHA NIMETIMIZA MASHARTI

Ili kuthibitisha umetimiza masharti, afisa wa uchaguzi anapaswa kuthibitisha usajili wako. Ikiwa umejiandikisha, unaweza kupiga kura. Wagombeaji walio kwenye kituo cha kupigia kura hawapaswi kuzungumza moja kwa moja na wapiga kura au kutatiza upigaji kura. AFISA WA UCHAGUZI PEKEE NDIYE AMERUHUSIWA KUKUULIZA UTHIBITISHE USAJILI WAKO AU UONYESHE KITAMBULISHO CHAKO.

HAKI ZANGU NI ZIPI?

Una haki ya: Kupokea usaidizi kutoka kwa mtu unayemchagua, isipokuwa mkuu wako au mwakilishi wa chama, Kupata karatasi mpya ya kura ikiwa umekosea, Kupiga kura kando ya gari lako ikiwa huwezi kuingia kituoni, Kupiga kura bila vitisho, ikiwemo vitisho kutoka kwa polisi, waangalizi wa kura, au wapinzani. Hakuna anayeruhusiwa kuvuruga kituo cha kura au kuzuia watu kuingia. Ripoti vitisho vyovyote mara moja kwa wasimamizi wa kura na upige Simu kwa Huduma ya Dharura ya Ulinzi wa Uchaguzi kupitia nambari 1-866-OUR-VOTE.

KUTOFIKA KUPIGA KURA

Angalia Kadi ya MOVPC "Understanding Absentee Voting" ili upate Maelezo Zaidi Ikiwa kura yako uliyotuma kupitia posta imepotea, imeharibika, au haijafika kwenye ofisi ya uchaguzi, bado unaweza kupiga kura kwenye uchaguzi!!

Je, huna kura? Jaza Hati ya Kiapo ya Kupotea kwa Kura kisha upige kura maalum kabla ya Siku ya Uchaguzi au kura ya kawaida (ya kuhesabiwa papo hapo) Siku ya Uchaguzi. Una kura yako? Peleka kura yako kituoni na upige kura huko. Huwezi kuwasilisha kura maalum kwenye kituo cha uchaguzi

Mpya: Mtu yeyote anaweza kutumia Kitambulisho kupiga kura mapema kwa kufika kituoni wiki 2 kabla ya Siku ya Uchaguzi

Je, una maswali au unahitaji usaidizi? Piga simu au tuma ujumbe kwa
1-866-OUR-VOTE
(1-866-687-8683)

Gumzo la Mtandaoni: 866OURVOTE.org Huduma za Lugha Mahususi: Kihispania 888-VE-Y-VOTA • Lugha za Asia 888-API-VOTE • Kiarabu 844-YALLA-US

1-866-OUR-VOTE